JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BENKI KUU YA TANZANIA

**07 Agosti 2025**

## TAARIFA KWA UMMA

## KUANZISHA UTARATIBU WA USIMAMIZI BINAFSI KWA TAASISI ZA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA ZA DARAJA LA PILI

Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kwa kushirikiana na Chama cha Taasisi za Huduma Ndogo za Fedha (TAMFI) pamoja na Umoja wa Taasisi za Huduma Ndogo za Fedha (TAMIU) inapenda kutangaza rasmi kuanza kwa utaratibu wa ushirikiano wa kimkakati unaolenga kuboresha nidhamu ya kujisimamia na mwenendo wa soko katika sekta ya watoa huduma ndogo za fedha nchini.

Miongoni mwa juhudi endelevu za kuimarisha ulinzi wa watumiaji wa huduma za fedha na kuboresha usimamizi kwa watoa huduma ndogo za fedha wa daraja la pili, Benki Kuu imeamua kutumia utaratibu wa usimamizi binafsi kwa kushirikiana na vyama vya watoa huduma ndogo za fedha. Utaratibu huu umeundwa ili kukamilisha mfumo wa sasa wa usimamizi wa Benki Kuu kwa kutumia uwezo wa vyama hivyo katika kufikia wanachama wao.

Kupitia ushirikiano huu na kwa kuzingatia mamlaka ya kisheria ya Benki Kuu ya Tanzania:

- Vyama vya Watoa Huduma Ndogo za Fedha (TAMFI na TAMIU) vimepewa rasmi jukumu la kuwa Taasisi zinazotumia Mbinu Elekezi Kujidhibiti, zenye wajibu wa kukuza na kusimamia mwenendo bora wa soko, utatuzi wa migogoro, na utekelezaji wa mbinu bora miongoni mwa wanachama wao.

- Benki Kuu itaendelea kutoa leseni kwa Taasisi za Watoa Huduma Ndogo za Fedha wa Daraja la Pili, kusimamia utekelezaji wa jumla na kusaidia TAMFI na TAMIU katika kuzingatia makubaliano yao, ili kuhakikisha wanaotoa



16 Barabara ya Jakaya Kikwete, S. L. P. 2303, 40184 Dodoma – Tanzania
Email: governoroffice@bot.go.tz Website: www.bot.go.tz, Simu: +255 22 223 2000/3000/3215/2501
Simu ya Mezani +255 22 223 3021/3022

huduma hizo wanajisimamia kwa kuzingatia masharti ya leseni zao, hivyo kuhakikisha utekelezaji mzuri na uzingatiaji wa viwango vya kisheria na vya kikanuni.

- Taasisi zote za Huduma Ndogo za Fedha za Daraja la Pili zinalazimika kujiunga na TAMFI au TAMIU ndani ya kipindi cha miezi sita tangu tarehe ya taarifa hii na kuzingatia makubaliano ya kujisimamia kwa kupitia utaratibu huu.

Utekelezaji wa utaratibu huu unaonesha dhamira ya pamoja ya kuboresha mazingira ya Watoa Huduma Ndogo za Fedha ili yaaminike, yawe wazi na rafiki kwa watumiaji wa huduma hizo. Hivyo, Benki Kuu inawahimiza wadau wote na umma kwa ujumla kuunga mkono na kushiriki kikamilifu katika mpango huu muhimu wa kuendeleza ujumuishaji wa kifedha na kukuza mfumo imara wa Watoa Huduma Ndogo za Fedha nchini.

Emmanuel M. Tutuba
**GAVANA**

,



16 Barabara ya Jakaya Kikwete, S. L. P. 2303, 40184 Dodoma – Tanzania
Email: governoroffice@bot.go.tz Website: www.bot.go.tz, Simu: +255 22 223 2000/3000/3215/2501
Simu ya Mezani +255 22 223 3021/3022